



# OFISI YA MUFTI WA TANZANIA

**KISWAHILI –KINGEREZA  
MSINGI WA KUJUA KUSOMA, KUONGEA NA KUZUNGUMZA  
KIINGEREZA**

**ENGLISH**  
LANGUAGE

INFORMATION  
STUDENT TEACH  
TRAVEL FOREIGN LEARNING  
ENGLAND TEACHER



**HATUA YA KWANZA**

[www.bakwataonlineacademy.ac.tz](http://www.bakwataonlineacademy.ac.tz)

UTANGULIZI .....	4
Mbinu za kujifunza lugha hususani lugha ya English.....	4
1. Kudhamiria kuweza: .....	4
2. Kujiwekea muda maalum wa kufikia kiwango fulani :.....	4
3.Kusoma kwa mpangilio:.....	5
4. Kusoma kwa mfululizo bila kukatisha:.....	5
5. Kufahamu matumizi ya nyakati na kanuni zake : .....	5
Lesson 1a .....	6
GREETINGS.....	6
(Salamu).....	6
A.Common greetings –(salamu za kawaida) .....	6
These greetings are six: .....	6
B. Other greetings – Salamu nyingine .....	8
Lesson 1b: Classroom Instructions .....	11
Classroom Instructions [maagizo ya darasani] .....	11
Lesson 2a: .....	13
Greetings.....	13
Lesson 2b: .....	17
Other Forms of Greetings .....	17
Lesson 2c:.....	18
Respectful Terms That .....	18
Accompany Greetings.....	18
Lesson 3: .....	19
Classroom Vocabulary .....	19
Question Formation.....	21
Lesson 4: .....	21
Personal Pronouns.....	21
Lesson 5: .....	25
Possessive Pronouns.....	25
Lesson 6: .....	27
School Subjects .....	28
Lesson 7a .....	32
Continents.....	32
Lesson 7b: .....	33
Countries.....	33
Lesson 7c:.....	36
Nationality .....	36

Lesson 7d: .....	39
Languages .....	39
Lesson 8: .....	41
Locations.....	41
Lesson 9: .....	44
Swahili Noun Classes.....	44
Lesson 9a: .....	46
Noun Classes.....	46
Lesson 9b: .....	52
Noun Classes.....	52
Lesson 9c.....	56
Noun Classes.....	56
Lesson 9d: .....	61
Noun Classes.....	61
D). Majina ya vitu ambavyo havihesabiki .....	65
[nouns of things that cannot be counted, which exist only in the plural form.....	65
Lesson 9e: .....	67
Noun Classes.....	67
Lesson 9f: .....	73
Noun Classes.....	73
C). Nouns that are mostly formed from adjectives, .....	76
nominals, or verbal roots.....	76
Lesson 10: .....	78
Family.....	78
Lesson 11: .....	85
The Verb -NA.....	85
Lesson 12 .....	87
Various Personalities .....	87
Various Personalities [watu mbalimbali] A). Various.....	87
Question Formation .....	95
Lesson 12b .....	98
Various Professions.....	98
Various Professions [kazi mbalimbali] .....	98
Lesson 13: .....	100
Tenses .....	100
B). Present Perfect [wakati uliopo hali timilifu] .....	101
Lesson 14a: .....	103
Numbers and Counting .....	103
Numbers and Counting [nambari na hesabu].....	103
FINAL EXAMINATION .....	109

## UTANGULIZI

### Mbinu za kujifunza lugha hususani lugha ya English.

#### 1. Kudhamiria kuweza:

Usianze au kuendelea kujifunza kiingereza bila kujiaminisha na kudhamiria kuweza haswa kwa ufasaha. Haitoshi tuu kutamani kuweza kiingereza, unahitaji nguvu ya dhamira ya toka moyoni , na kujiaminisha kuwa wewe unaweza.

#### 2. Kujiwekea muda maalum wa kufikia kiwango fulani :

Haitoshi tuu kudhamiria kuweza kuongea lugha ya kiingereza. Unahitaji kujiwekea malengo na mikakati ya kufikia hilo lengo na iwe kufikia lengo fulani ndani ya muda maalum.

Njia bora ya kujiwekea muda ni kuligawa lengo lako la kufahamu lugha katika vipengele vidogo vidogo halafu unaweka malengo ya kufanikisha hivyo vipengele vidogo vidogo ndani ya muda fulani.

Kwanza fahamu picha kubwa ya yote unayotakiwa kujifunza, kisha jiulize yapi kati ya hayo tayari unayajua au pengine una 'idea' nayo.

Hivyo weka malengo kwa kila kipengele kuendana na uwezo wako wa kuelewa.

Mfano ukishajua vipengele vyote mfano vya TENSES, jiulize ndani ya muda gani utaweza kukamilisha tenses. Hivyo hivyo kwa vipengele vingine .

Kutambua viungo mbalimbali vinavyounda sentensi:

Kila unachoandika, kuongea, kusikia au kusoma ni SENTENSI. Katika sentensi unaandika, kusoma, kusikiliza au kuongea maneno. Hata hivyo ili kurahisisha watu kujifunza lugha, maneno hayo yamegawanywa katika makundi , na hayo makundi yanafafanua matumizi na kanuni kuhusu kila neno katika kundi husika.

*Mfano sentensi hii : Will you come to school ? - Je utakuja shule ?*

Hapa tuna maneno matano, na yanatoka katika makundi yafuatayo:

Verbs: Will na Come

Pronoun: You

Proposition: TO

Noun: School

Kufahamu kanuni zinazoongeza makundi haya zitakafunya ujue kwanini hayo maneno yamepangiliwa hivyo yalivyo , mfano kwanini haikuwa COME WILL TO SCHOOL YOU ?

Katika kujifunza kanuni hizi ndipo utakapojitofautisha wewe na wale ambao wanadhani kujifunza lugha ni kujua maneno mengi.

Kuna watu wengi wanajua maneno mengi ya kiingereza na ni wepesi wa kuchanganya kiswahili na kiingereza wakati wa mazungumzo ila inapofika kuongeza kiingereza tuu kwa mfululizo inakuwa ni tabu kwakuwa hawana ujuzi wa kuunda vema sentensi.

### **3. Kusoma kwa mpangilio:**

Baada ya kufahamu kuwa lugha ina vipengele kadhaa vinavyounda sentensi na kanuni zinazoongoza kila aina ya maneno , bila kusahau nyakati –tenses, jiwekee utaratibu wa kusoma hatua kwa hatua kwani vipengele vingi vinaendana.

Mfano kama haujalewa vizuri tenses, itakupa shida kuelewa active and passive voice, na reported speeches.

### **4. Kusoma kwa mfululizo bila kukatisha:**

Mbinu nyingine ni kuhakikisha kuwa unajifunza lugha kwa muda maalum na kwa mfululizo. Sio unajifunza kwa "manati" mara moja au mbili tuu ndani ya mwezi. Ili kufanikiwa kujifunza kwa urahisi na kwa haraka hakikisha unatenga muda walau mara tatu kwa wiki, na kwa muda wa walau masaa mawili kila siku na hakikisha unasoma hivi kwa muda mrefu mfano walau kwa miezi mitatu mfululizo kwa kasi hiyo hiyo ya kujifunza.

Kwanini unahitaji kujifunza kwa mfululizo ? Ni kwa sababu kujifunza lugha kunahitaji sana kukumbuka na kuhusanisha uelewa wa vipengele tofauti vya lugha.

Hivyo kujifunza mfululizo kunatuma ujumbe kwa ubongo wako kuwa hayo unayotaribu kuhifadhi katika kumbukumbu yako ni ya muhimu, hivyo nao unatenga nafasi ya kukusaidia kuyapata haraka unapohitaji –yaani kumbukumbu ya haraka.

Kumbuka pia hata kama unasoma na yanakua magumu, ukiendelea kurudia mara kwa mara jambo lile lile baada ya muda unajikuta umeshajenga aina fulani ya kumbukumbu na uwezo wa kuhusanisha yale uliyojifunza zamani na taarifa mpya ya jambo hilo hilo husika.

### **5. Kufahamu matumizi ya nyakati na kanuni zake :**

Mbinu hii inahusu vitu viwili muhimu sana, kwanza kujua uwepo wa nyakati na matumizi yake yaani je katika hali ipi unatumia present tense, au past tense, au future tense, halafu kitu kingine cha pili cha muhimu sana ni kujua kanuni zinazoongoka namna ya utungaji wa sentensi katika kila aina ya nyakati.

## Lesson 1a

### GREETINGS

#### (Salamu)

Tunatamka(griitings)

#### What is it? (Ni nini )

This is how to know the condition of someone or something by saluting /salutation.

(Ni naman ya kujua hali ya mtu au kitu Fulani kwa kusalimiana/kuamka ).

So , we can say “ greetings “ is maamkizi or salamu in Kiswahili.

The word “greetings”comes from the word “greet” which means “ Salamu/amkia” in Kiswahili. (Neno “greetings” linatokana na neoni “ greet” ambalo ilina maana ya “salimu” au ‘amkia’ katika Kiswahili.)

#### Kinds of greetings: ( Aina za maamkizi /salamu )

There are two major kinds of greetings:

Kuna aina mbili za salamu

- a) Common greetings.( Komoni griitings )- ( salamu za kawaida)
- b) Other greetings. (adha griitings)- (salamu nyinginezo)

#### A.Common greetings –(salamu za kawaida)

They are greetings which you greet a person whom you hear his voice directly, whether by seeing him and listening his voice or by just listening his voice or by writing directly.

(Ni salamu ambazo unamsalimia mtu ambaye unaisikia sauti yake moja kwa moja , ama kwa kumwona na kumsikia au kwa kumsikia tu, au kwa kuandika moja kwa moja.)

#### These greetings are six:

- a )Good morning – Asubuhi njema / Habari za asubuhi.
- b) Good afternoon- Mchana mwema / Habari za mchana .
- c) Good evening – Jioni njema / Habari ya jioni
- d) Good night—Usiku mwema / Habari ya usiku.
- e) How do you do –Unaendeleaje na hali yako kwa kipindi kirefu / tangu tulipoachana.
- f) How do you feel – Unajisikiaje .

In these six common greetings ;three greetings resemble in responding , that is in answering.

The greetings which resemble in responding are : Good morning, Good afternoon and Good evening. This can be shown below by a chart which shows how to greet and how to answer / respond.

Katika salamu hizi sita za kawaida , salamu tatu hufanana katika kujibu, salamu ambazo hufanana katika kuitikia kujibu ni : Good morning, Good afternoon and Good evening . Hii inawezekana kuonyeshwa katika chati inayoonyesha namna ya kuitikia hapo chini.

We shall only pick one greeting from the three and show how we greet and how we respond.

Tunachukua salamu moja tu kutoka katika hizo tatu na tutaonyesha namna tunavyo salimu na kuitikia .

Let us now take “Good morning”  
Hebu sasa tuchukue “Good morning”

<b>Greeting</b>	<b>Response</b>
1. Good morning  a) (Kama ni mzima utajibu)  (Ayem fain /Ayem okei/ fain)	Good morning , how are you?  (Hawayuu)  Mjibu kama alivyojibu yeye  (Answer as he has answered)
b) (Kama siyo mzima utajibu)  I am not fine / I am not okay  (Ayem noti fain/ Ayem noti okei)	
c) Halafu mjulie nay eye hali yake tena  How are you too?  (Hawayuu tuu?)  Au How about you?  (Hau about yuu?)  Au and you ? (Endi yuu?) Maana yake , na wewew hali yako vipi	-I am also fine (Nami pia mzima)  -I am also fine.  (Nami pia mzima)  Au I am not fine (mimi si mzima)

(Haya majibizano kuanzia pale ambapo neno ‘how are you’ lilipotajwa na kuendelea yatatumiwa na salamu hizo zote tatu kujibizana , yaani salamu ya Good morning, Good afternoon and Good evening).

Now let us see the remaining greetings:  
(Sasa hebu tuone kwa salamu zinazobaki)

### **Good night**

Good night?	1. Good night to you
-Usiku mwema	-Usiku mwema na wewe

	(hapa basi hatuungezi tena chochote) 2.The same to you (Na wewe pia)
--	---

### How do you do?

Greeting	Responding
How do you do?  (hau du yuu duu)  Unaendeleaje na hali yako tangu tulipoachana ?	How do you do too (hau du yuu duu tuu)  NB. Hapo imekwisha (hatuungezi tena chochote)

### How do you feel?

Greetings	Responding
How do you feel ?  (hau du yuu fil?)  -Unajisikiaje	(kama unajisiikia vizuri,itikia ;  I feel alright /okay/fine  (Ai filorait/okei/fain)  Kama unajisikia vibaya, itikia ;  I don't feel alright/Okay/fine  (I donti filorait/ okei/fain)

### B. Other greetings – Salamu nyingine

These are greetings which you greet someone or something out of the one you speak to (or hear his voice ), but you want the one who speaks with you to answer on behalf.

(Hizi ni salamu unazomsalimu mtu Fulani au kitu flano nje ya Yule unayeongea naye au kumsikia sauti yake ,bali unataka yeye unayeongea aye ajibu kwa niaba )

Example: How about your sister?

Mfano: Hajambo dada yako?

Au (yu hali gani dada yako)

- (Hapa utaona huyo dada yuko nje ya unayetaka azijibu hizo salamu .Maana yake unataka kujua hali ya mtu au kitu au mnyama ambaye huonani naye wakati huo).

Generally, these kinds of greetings start with the word “how”

Mara nyingi ghizi salamu huanza na neon “how’

Mfano;HHow about John ? au How is your mother/ au How are they at home? N.k



( Sasa unaposema ‘How is.....’ maana yake unataka kumsalimia mtu au kitu kimoja;lakini ukisema ‘How are.....’, Maana yake unatka kuwasalimia watu wengi au vitu vingi au wanyama wengi.Lakini unaposema ‘How abouy.....”, hapa unaweza kusalimu wengi (Oplural names0 au mmoja (singular names) Watu wengi hupenda kutumia ‘How about.....’, maana ni rahisi na haitatanishwi.Pia ni multipurpose (maltiparpas)- maana inaweza kutumika kwa makusudi zaidi ya moja .)

Now let us see them at work

Sasa tuzione zifanyavyo kazi

Greeting	Answer/Responding
<p>1 .How is it? (hau iz it?) -Hali vipi?(Pia inaweza ikatumika unaposalimu kitu au mnyama baada ya kumtaja kwanza )mfano B: Nimemwona ng’ombe wako shambani  A.How is it? B:(Anajibu)- It is fine au it is not fine</p>	<p>Kama hali ni nzuri  -It is fine  Kama hali si nzuri  -It is not fine</p>
<p>2 .How things? (hau things)  -Mambo vipi?</p>	<p>-Fine (Kama ni mzuri)  -Not fine(kama ni mbaya)</p>
<p>3.How is he? (Hau iz hii?0- Hujambo? N.B Anayesalimiwa hapa ni mwanaume (kama ni mwanmke tungesema:How is she?) Hizi salamu mbili unamsalimia mtu baada ya kuwa mmekwisha mzungumzia kwanza kwa kumtaja jina.Kama hamjamzungumzia kwa kumtaja jina na unatka kumsalimia basi weka jina lake kabisa , Mfano : How is Asha/ au How is John?</p>	<p>(Kama ni mzima hapa unaitikia hivi:  He is fine  (kwa mwanaume) au She is fine (kwa mwanamke) (Kama hali yao mbaya utasema)  -He I not fine au -She is not fine</p>
<p>4.How is your brother?  Au How about your brother? ( hau abauti yua bradha?)  Hajambo kaka yako? Pia unaweza kuweka jina linguine lolote la</p>	<p>Unapojibu,unachofanya ni kuchunguza huyo anayesalimiwa ni mwanaume au mwanamke? Kama mwanaume unajibu  He is fine na kma ni mwanamke</p>

kingugu au kikazi mfano  Mother,Uncle, Aunt,Wife,Husband. (Haya ni ya kindugu ya kikazi kama Teacher, Boss, Manager, etc	She is fine na kinyume chake
--	------------------------------

5.How are your brothers?  (Hau aa yua bradhaz?)  Au How about your brothers? (Hau abauti yua bradhaz?)  Kaka zako hawajambo	Unapojibu salamu kama hii inayosolimia majina ya uwingi huwa tunatumia kiwakilishi 'They'  Mfano hapa tutaitikia hivi They are fine (dhei aa fain)  -Hawajambo  AU They are not fine (dhei aa noti fain) -Si wazima /hali yao si nzuri
--	--

-(Ina maana 'hawajambo?' Jambo la kuangalia hapa ni kwamba unaposolimia kwa kutumia pronoun (kiwakilishi cha jina kama 'They' inataiwa hao watu wazungumzwe kwanza (tena kwa majina) mfano;Nimekutana na Jane na Asha mjini leo.( sasa kama hivi majina yamkwishatajwa na tunataka kufahamu halizao ndipo tunatumia kiwakilishi cha hayo majina cha uwingi ambacho ni 'they' .Hivyo tunaema :How are they ? Lakini pia tunaweza kusema hivi;'Ho w are they at home au at Sinza " n.k

N.B:

You can also put other names as above , but those names must be in plural names.

-Unaweza pia (badala ya brothers) ukaweka majina mengine ya uwingi kwa sababu umetumia neon 'are' ambalo limetumiwapo hpo huita jina lililo katika uwingi kama Mothers,Children, Men, Girls etc)

N.B:

Tunapotumia 'about' hatuwek

i 'are' wala "is" Pia salamu hii tunaweza kusema hivi 'How are they ? tukiwa wengi.

6 .Hata hivyo tunaweza pia tukasalimia kazi, biashara , masomo,nyumbani,shambani, n.k kwa kusema tu :-  How are about home? au How about business? Au How about studies? Au How about your condition? (kondisheni)	-Hapa utajibu kulingana na jina lililotajwa kama ni plural au singular; kama ni la kike au la kiume au kama ni kitu au mnyama, Mfano:He is fine, She is fine ,They are fine au It is fine au ukajibu kwa jina lenyewe .  Majibu yake yatategema jinsia ya huyo ambaye anauliziwa
---	--

N.B:	
Condition maana yake 'Hali au pia unaweza ukatumia 'situation'.(stueshen)	

Pia unaweza kumsalimia mtu mwingine ambaye anahusiana na mtu mwingine ambaye yuko nje ya Yule tunaye onga naye .Mfano:tunataka kusalimu hivi :Hajambo mke wa kaka yako? Au Hajambo mwalimu wa binti yako? Au Hajambo rafiki wa dada yako/ au Vipi hali ya garila babu yako?.

- a ) How about your brother's wife? au
- b ) How about your daughter's teacher? au
- c )How about your sister's friend? Au
- d ) How about your father's car ? N.K

La msingi hapa tusingahau kuweka koma juu ya 'S' na juu ya herufi ya mwisho ya jina la huyo anae mmiliki.

Hapa jibu lake ni lile la:

-Are fine (kama ni wazima ) au

-Are not fine (kama si wazima )

-Hapa utajibu kulingana na jina lililotajwa : kama ni plural au singular ; kama ni la kike au la kiume au kama ni la kitu au mnyama ,mfano:

-Majibu yake yanategemea jinsia ya huyo amabaye hali yake inaulizwa.

## Lesson 1b: Classroom Instructions

### Classroom Instructions [maagizo ya darasani]

rudia	repeat
mwalimu	teacher
profesa	professor
mwanafunzi	student
jibu	answer; respond
uliza	ask
unaelewa?	do you understand?
mnaelewa?	do you all understand?
ndiyo	yes
la; hapana	no
swali	question
mna swali?	does anyone have a question?
mwalimu, nina swali	teacher, I have a question
sielewi	I do not understand
sikiliza	listen (s. command)
sikilizeni	listen (pl. command)
simama	stand
tafadhali, simama	please, stand

keti; kaa	sit
tafadhali, keti/kaa	please, sit down
kusanya	collect
karatasi	paper
tafadhali, kusanya karatasi	please, collect the papers
leta	bring
tafadhali, leta karatasi	please, bring the papers
enda	go
tafadhali, enda	please, go
tazama	look
funga kitabu	close the book
fungua kitabu	open the book
tafadhali	please
tafadhali rudia	please repeat
tafadhali, fungua kitabu	please, open the book
tafadhali, nyamaza	please, be quiet (sing.)
tafadhali, nyamazeni	please, be quiet (pl.)
tafadhali, ongea/zungumza/sema katika Kiingereza	please, speak in English
tafadhali, jibu katika/kwa Kiswahili	please, respond in Kiwahili
tafadhali, ongea/zungumza/sema katika Kiswahili	please, speak in Kiwahili
polepole	slowly
tafadhali, ongea/zungumza/sema polepole	please, speak slowly
taja	mention
tamka	pronounce
soma	read; study
andika	write

## Lesson 1: Classroom Instructions

andika kwa Kiswahili	write in Kiwahili
tafadhali soma	please read
kumbuka	remember (sing.)
mnakumbuka	remember (pl.)
jaribu	try
tena	again
jaribu tena	try again
tafadhali jaribu	please try
karibu	welcome
tafadhali fungua mlango	please open the door
tafadhali fungua mlango	please close the door
tafadhali kaa/keti	please sit (sing.)
"Crying" ni nini kwa Kiswahili?	What is "crying" in Kiwahili?
tafsiri	translate
chemsha bongo	brain teaser
sijui	I do not know
kwaheri	bye
kwaheri, tutaonana kesho	goodbye, hope to see you tomorrow
kwaheri, tutaonana baadaye	goodbye, hope to see you later
asante	thank you
asante sana	thank you very much
njoo	come
tafadhali, njoo	please, come
samahani	pardon; excuse me
samahani, mwalimu, nina swali	excuse me, teacher, I have a question
haraka	fast
tafadhali, ongea/zumgumza/sema	
haraka haraka	please, speak quicker
vizuri	good
vizuri sana	very good
Wewe ni mzuri.	You are good.
Wewe ni mbaya.	You are bad.
kazi nzuri	good work
kazi ya nyumbani	homework
Leo tutasoma _____.	Today we will learn _____.
Jana tulisoma nini?	What did we learn/study yesterday?
Leo tumesoma nini?	What have we learned/studied today?

## Lesson 2a:

### Greetings

#### Greetings [maamkio; salamu]

There are at least five ways of greeting in Kiswahili:

**A).** Habari gani?

- B). Hujambo?
- C). U hali gani?
- D). Shikamoo.
- E). Mambo? / Vipi?

A). Habari gani?

Example 1 - *Two people greeting each other*

Person A: **Habari gani?**

Person B: **Nzuri!**

Sentensi:

a). Nzuri / njema / salama / safi / sawa / poa. [Good / nice / peaceful / clean / fine / cool.]

b). Nzuri / njema / salama / safi / sawa / poa **sana...**

[**Very** good / nice / peaceful / clean / fine / cool.] c). Nzuri / njema / salama / safi / sawa / poa **tu...**

[**Just** good / nice / peaceful / clean / fine / **just** cool.]

B). Hujambo?

Example 2 - *Teacher greeting students*

Example 1 - *Two people greeting each other*

Person A: **Hujambo?**

Teacher: **Hamjambo?**

Person B: **Sijambo!**

Students: **Hatujambo!**

Sentensi:

Hujambo? [Any issue(s)? / *How are you doing?*]

Sijambo! [No issue(s)! / *I am okay/fine!*]

Hamjambo? [Any issue(s)? / *How are you doing?*]

Hatujambo! [No issue(s)! / *We are okay/fine!*]

### C). U hali gani?

Example 1 - *Two people greeting each other*

Person A: **U hali gani?**

Person B: **Njema.**

Example 2 - *One person greeting many people*

Person A: **M hali gani?**

Persons B, C, & D: **Salama.**

Sentensi:

1. U hali gani? / M hali gani?

What's your condition? / *How are you?*]

a). Nzuri / njema / salama / safi / sawa / poa. [Good / nice / peaceful / clean / fine / cool.]

b). Nzuri / njema / salama / safi / sawa / poa **sana...**

[**Very** good / nice / peaceful / clean / fine / cool.] c). Nzuri / njema / salama / safi / sawa / poa **tu...**

[**Just** good / nice / peaceful / clean / fine / **just** cool.]

### D.) Shikamoo.

Example 1 - *A youth greeting an elder person*

Youth: **Shikamoo.**

Elder Person: **Marahaba.**

Sentensi:

Shikamoo. [I touch your feet.]

Marahaba. [I am delighted.]

### E). Vipi? / Mambo?

Example 1 - *A youth greeting another youth*

Youth A: **Vipi?**

Youth B: **Poa.**

Example 2 - *A youth greeting another youth*

Youth A: **Mambo?**

Youth B: **Safi.**

Sentensi:

Vipi? / Mambo? [What's up?]

Poa / Safi / Sawa. [Cool / Clean / Fine.]

Mifano:

<b>1.</b> Hodi!	[Requests permission to enter a house.]
<b>2.</b> Karibu!	[Welcome!]
<b>3.</b> Karibu ndani!	[Welcome inside!]
<b>4.</b> Asante.	[Thank you.]
<b>5.</b> Asante sana.	[Thank you very much.]
<b>6.</b> Kwaheri.	[Be blessed. / Goodbye.]
<b>7.</b> Tutaonana baadaye.	[We will see each other later.]
<b>8.</b> Habari za asubuhi/ mchana/jioni/usiku?	[How is the news of the morning/afternoon/evening/night?]
<b>9.</b> Habari za mama/baba/kaka/dada/ ndugu/mjomba	[How is the news of mother/father/brother/sister/comrade/uncle]
<b>10.</b> Habari za nyumbani/shuleni/chuoni/ masomo/Amerika	[How is the news at home/at school/at college/studies/America]



## Lesson 2b:

### Other Forms of Greetings

#### Greetings

##### Mifano:

Waambaje?	[How are you doing?]	Sina la kuamba. [I have nothing to say.]
Salaamaleikum.	[Peace be upon you.]	Aleikumsalaam. [And also with you.]
Upo?	[Are you there?]	Nipo. [I am here.]
Lala salama.	[Sleep peacefully.]	Nawe pia. [And you also.]
Tuonane kesho.	[See you tomorrow.]	Inshallah. [God willing.]
Ndoto njema.	[Dream well.]	Za mafanikio. [Of success.]
Lala unono.	[Sleep comfortably.]	Nawe pia. [And you also.]
Usiku mwema.	[Good night.]	Wa buraha. [With tranquility.]
Usingizi mwema. [Sleep well.]		Wa buraha. [With tranquility.]
Habari za kutwa? [How was your day?]		Njema/Nzuri. [Good.]
Jioni njema.	[Good Evening]	Salama! [Peaceful!]
Uende salama	[Go with peace.]	Tuonane inshallah! [We will see each other God willing]

## Lesson 2c:

### Respectful Terms That

#### Accompany Greetings

<b>Respectful Terms</b>	Salamu, Adabu, Heshima , Tafside [Peace, Politeness, Honorable, Civil]
Mifano:	

Samahani	[Excuse me]
Niwe radhi	[My apologies/Pardon me]
Tafadhali	[Please]
Pole	[Sorry]
Makiwa	[Term used to express condolences]
Asante	[Thank you]
Heko/Hongera	[Congratulations]
Shukrani	[Thanks]
Inshallah	[God willing]
Binti	[Daughter of]
Bin	[Son of]
Bi/Biti	[Miss/Ms.]
Bibi	[Mrs.]
Bwana	[Mr./Sir]
Marehemu	[The late]
Bimdogo	[Little miss / young lady]
Bwanamdogo	[Little sir / young man ]
Bimkubwa	[Middle aged/ elderly woman]
Bwanamkubwa	[Middle aged / elderly man]]
Hayati	[Distinguished deceased person]
Ustadh	[Distinguished scholar]
Guru	[Spiritual leader / expert/innovative person]

## Lesson 3:

### Classroom Vocabulary

#### Classroom Vocabulary [msamiati wa darasani] A). Vocabulary

mlango / milango	[door/ doors]
dirisha / madirisha	[window / windows]
taa / taa	[light / lights]
ubao / mbao	[board / boards]
kompyuta / kompyuta	[computer / computers]
kiti / viti	[chair / chairs]
meza / meza	[table / tables]
kalamu / kalamu	[pen / pens]
penseli / penseli	[pencil / pencils]
mkoba / mikoba	[bag for books / bags for books]
mfuko / mifuko	[bag of books / bags of books]
kitabu / vitabu	[book / books]
daftari / madaftari	[notebook / notebooks]
kabati / makabati	[cupboard / cupboards]
rula / rula	[ruler / rulers]
ufutio / futio	[eraser / erasers]
wino / wino	[ink / inks]
ukuta / kuta	[wall / walls]
sakafu / sakafu	[floor / floors]
dari / dari	[ceiling / ceilings]
paa / paa	[roof / roofs]
simu / simu	[telephone / telephones]
karatasi / karatasi	[paper / papers]
jaa / jaa	[litter bin / litter bins]
chaki / chaki	[chalk / chalks]
zulia / mazulia	[carpet / carpets]
swichi	[switch]
swichi ya feni	[fan switch]
swichi ya taa	[light switch]

mwanafunzi / wanafunzi	[student / students]
mwalimu / walimu	[teacher / teachers]
kalenda/kalenda	[calendar / calendars]
saa / saa	[clock / clocks]
saa ya ukuta	[wall clock]
ramani / ramani	[map / maps]
kiyoyozi / viyoyozi	[air conditioner / air conditioners]
picha / picha	[picture / pictures]
mchoro / michoro	[drawing / drawings]
pazia / mapazia	[curtain / curtains]
runinga/televisheni	[television / televisions]
video/video	[video / videos]
kengele / kengele	[bell / bells]
chati / jedwali	[chart / charts]
rejesta / rejesta	[register / registers]
bendera / bendera	[flag / flags]
bendera ya taifa	[national flag]
kengele / kengele	[bell / bells]
mlinzi / bawabu / walinzi	[security / security]
saa / saa	[clock / clocks]
saa ya ukuta	[wall clock]
chati / jedwali	[chart / charts]
ramani / ramani	[map / maps]
kalenda / kalenda	[calendar]
rejista / rejista	[register / roll call]
majilisi / masjala / ofisi	[office / staff room]
picha / picha	[picture/ pictures]
deski / dawati	[desk]
gazeti / magazeti	[newspaper / newspapers]
jarida / majarida	[journal / periodical]
habari / habari	[news]
barua / barua	[letter / letters]
makala / makala	[article / articles]
insha / insha	[essay / essays]
kumbukumbu / kumbukumbu	[record / records]
kabrasha / ripoti maalum	[pamphlet / meeting documents]

## Question Formation

Mifano:

### 1. Darasa hili lina vitu gani?

[What things does this classroom have?]

Darasa hili lina meza, mkoba, chaki, ubao...

[This classroom has a table, backpack, chalk, board...]

### 2. Hii ni nini?

[What is this?]

Hii ni meza.

[This is a table.]

### 3. Huu ni nini?

[What is this? (referring to wall)]

Huu ni ukuta.

[This is a wall.]

### 4. (Wewe) Hupendi mapambo gani? [Which decorations don't you like?]

(Mimi) Sipendi \_\_\_\_\_. [I don't like \_\_\_\_\_.]

## Lesson 4:

## Personal Pronouns

### Personal Pronouns [viwakilishi - nafsi]

There are three personal pronouns in Swahili:

- A). First person pronoun
- B). Second person pronoun
- C). Third person pronoun

Each personal pronoun has a singular and a plural form.

#### A). First Person Pronoun

Umoja [singular]

**Mimi** [I/Me]

Represented by **NI-**

Wingi [plural]

**Sisi** [We/Us]

Represented by **TU-**

Sentensi:

Mimi **ninaitwa** Jeremy.

[I am called Jeremy. / *My name is Jeremy.*]

Sisi **tunaitwa** Jeremy.

[We are called Jeremy. / *Our names are  
Jeremy.*]

B). Second Person Pronoun

<u>Umoja [singular]</u> <b>Wewe</b> [You] Represented by <b>U-</b>	<u>Wingi [plural]</u> <b>Nyinyi/Ninyi</b> [You (pl.)] Represented by <b>M-</b>
--	--

Sentensi:

Wewe **unaitwa** Jeremy.

[You are called Jeremy. / *Your name is Jeremy.*]

Nyinyi/Ninyi **mnaitwa** Jeremy.

[You (pl.) are called Jeremy. / *Your names are Jeremy.*]

C). Third Person Pronoun

<u>Umoja [singular]</u> <b>Yeye</b> [He/She, Her/Him] Represented by <b>A-</b>	<u>Wingi [plural]</u> <b>Wao</b> [They/Them] Represented by <b>WA-</b>
--	--

Sentensi:	
Yeye <b>anaitwa</b> Jeremy.	[He is called Jeremy. / <i>His name is Jeremy.</i> ]
Wao <b>wanaitwa</b> Jeremy.	[They are called Jeremy. / <i>Their names are Jeremy.</i> ]

### Muhtasari [Summary]

Nafsi [Personal Pronoun]		Kiwakilishi [Marker]
<i>1st Person:</i>		
<b>Mimi</b>	[I/Me]	<b>NI-</b>
<b>Sisi</b>	[We/Us]	<b>TU-</b>
<i>2nd Person:</i>		
<b>Wewe</b>	[You]	<b>U-</b>
<b>Nyinyi/Ninyi</b>	[You (pl.)]	<b>M-</b>
<i>3rd Person:</i>		
<b>Yeye</b>	[He/She, Her/Him]	<b>A-</b>
<b>Wao</b>	[They/Them]	<b>WA-</b>

### Zingatia [Note]

ita	[call]
itwa	[be called]
Ninaitwa ____ .	[I am called ____ . / <i>My name is ____ .</i> ]
Nani?	[Who?/What is his/her name?]
Na wewe je?	[And what about you?]

### Question Formation

Mifano: _____	<b>1. Wewe unaitwa nani?</b>
[What is your name?]	
Mimi <b>ninaitwa</b> Jeremy.	[I am called Jeremy / <i>My name is Jeremy.</i> ]
<b>4. Nyinyi mnaitwa nani?</b> [What are your names?]	
Sisi <b>tunaitwa</b> Jeremy.	[We are called Jeremy/ <i>Our names are Jeremy.</i> ]





### 3. Yeye anaitwa nani?

[What is he/she called? / *What is his/her name?*]

Yeye anaitwa Jeremy.

[He is called Jeremy / *His name is Jeremy.*]

### 4. Wao wanaitwa nani?

[What are they called? / *What are their names?*]

Wao wanaitwa Jeremy.

[They are called / *Their names are Jeremy.*]

### 5. Mimi ninaitwa John.

[I am called John]

Na wewe je?

[And what about you?]

Mimi ninaitwa Andrew.

[I am called Andrew.]

## Lesson 5:

## Possessive Pronouns

### Possessive Pronouns [vivumishi vimilikishi]

There are three possessive pronouns in Swahili:

A). First person possessive

B). Second person possessive

C). Third person possessive

Each possessive pronoun has a singular and a plural form.

#### A). First Person Possessive

Umoja [singular]  
-ANGU [my]

Wingi [plural]  
-ETU [our]

Mifano:

Mwalimu **wangu** [My teacher]

Mwalimu **wetu** [Our teacher]

Walimu **wangu** [My teachers]

Walimu **wetu** [Our teachers]

#### B). Second Person Possessive

Umoja [singular]  
-AKO [your]

Wingi [plural]  
-ENU [your (pl.)]

Mifano:

Kalamu **yako** [Your pen]

Kalamu **yenu** [Your (pl.) pen]

Kalamu **zako** [Your pens]

Kalamu **zenu** [Your (pl.) pens]

#### C). Third Person Possessive

Umoja [singular]  
-AKE [his/her]

Mifano:

Jina **lake** [His/her name]

Majina **yake**

[His/her names]

Wingi [plural]

**-AO [their]**

Jina **lao**

[Their name]

Majina **yao**

[Their names]

## Muhtasari [Summary]

<p><i>1st Person Singular:</i></p> <p style="text-align: center;"><b>-ANGU</b> [My]</p>	<p><i>1st Person Plural:</i></p> <p style="text-align: center;"><b>-ETU</b> [Our]</p>
<p><i>2nd Person Singular:</i></p> <p style="text-align: center;"><b>-AKO</b> [Your]</p>	<p><i>2nd Person Plural:</i></p> <p style="text-align: center;"><b>-ENU</b> [Your (pl.)]</p>
<p><i>3rd Person Singular:</i></p> <p style="text-align: center;"><b>-AKE</b> [His/Her]</p>	<p><i>3rd Person Plural:</i></p> <p style="text-align: center;"><b>-AO</b> [Their]</p>

## Zingatia [Note]

-angu	[my]
-ako	[your]
-ake	[his/her]
jina	[name]
langu	[my]
lako	[your]
lake	[his/her]
nani?	[Who? What is his/her name?]
ni	[is]

## Question Formation

Mifano:

### 1. Jina langu ni nani?

[What is my name?]

Jina lako ni Peter.

[Your name is Peter.]

### 2. Jina lako ni nani?

[What is your name?]

Jina langu ni Darnell.

[My name is Darnell.]

### 3. Jina lake ni nani?

[What is his/her name?]

Jina lake ni Don.

[His/her name is Don.]

### 4. Jina lako ni nani mama/mwalimu?

[What is your name, mom/teacher?]

## Lesson 6:

## School Subjects

### School Subjects

[masomo]

#### A). School Subjects

afya ja jamii	[community health]
akiolojia; elimu kale	[archeology]
anthropolojia	[anthropology]
bayolojia	[biology]
biashara	[business]
botania	[botany]
dini	[religion]
elimu	[education]
elimu ya kompyuta	[computer science]
elimu ya maktaba; ukutubi	[library science/studies]
elimu ya mazingira	[environmental science]
elimu ya mawasiliano	[communication studies]
elimu ya siasa	[political science]
elimu ya usimamizi wa fedha	[finance]
falsafa	[philosophy]
fasihi	[literature]
fizikia	[physics]
hisabati; hesabu	[math]
historia	[history]
isimu (ya lugha)	[linguistics]
jiografia	[geography]
jiolojia	[geology]
kemia	[chemistry]
Kihispania	[Spanish]
lishe	[nutrition]
lugha	[language]
masomo ya Kiafrika	[African studies]
masomo ya maendeleo	[development studies]
masomo ya wanawake	[women's studies]
matibabu ya watoto	[pediatrics]

meteorolojia  
mipango ya miji

[meteorology]  
[urban planning]

muziki	[music]
saikolojia	[psychology]
sanaa	[fine arts]
sanaa za maonyesho	[theater arts]
sayansi	[science]
sayansi kimu	[home economics]
sayansi ya jamii	[social science]
sayansi ya mimea	[plant science]
sheria	[law]
sosholojia	[sociology]
uandishi	[journalism]
uchumi	[economics]
uganga; udaktari	[medicine]
uhandisi	[engineering]
unesi	[nursing]
uongozi; manejimenti	[management]
upasuaji	[surgery]
usanifu majengo	[architecture]
utangazaji	[advertising]

#### Zingatia [Note]

Some academic subjects are expressed by using *elimu* or *masomo*. However, school subjects that are not listed with *elimu* or *masomo* could optionally be expressed by using the following structure: *elimu ya biashara*, *elimu ya dini*, *masomo ya dini*, *elimu ya uhandisi*, etc.

soma	[study]	Gani?	[What?/which?]
katika	[at/within]	Nini?	[What?]
chuo kikuu	[university]	Wapi?	[Where?]

Mifano:

**1. Wewe unasoma masomo gani?**[What subjects do you study? / *What do you study?*]

Mimi ninasoma historia.

[I study history.]

**5. Wewe unasoma nini?** [What do you study?]

Mimi ninasoma historia na kemia.

[I study history and chemistry.]

### 3. Wewe unasoma wapi? [Where do you study?]

Mimi ninasoma katika chuo kikuu cha Kansas.

[I study at the University of Kansas.]

How to introduce yourself and what you study:

Jina langu ni Sheila/Ninaitwa Sheila. Ninasoma historia katika chuo kikuu cha Kansas. Na wewe je?

[*My name is Sheila/I'm called Sheila. I study history at the University of Kansas. What about you?*]

## Lesson 7a

### Continents

#### Continents [Mabara]

#### A). Continents

Mfano:

Bara la Afrika / Bara Afrika	[African continent]
Bara la Ulaya / Bara Uropa	[European continent]
Bara Amerika Kusini	[South American continent]
Bara Amerika Kaskazini	[North American continent]
Bara Asia / Hindi	[Asian continent]
Bara Australia	[Australian continent]
Bara Antakitika	[Antarctica]



## Lesson 7b:

### Countries

#### Countries [nchi]

Countries take three different forms:



U-prefix

- Some change completely
- Some do not change at all

#### A). Countries

Marekani; Amerika	[USA]
Uingereza	[England]
Mashariki ya kati	[Middle East]
Misri	[Egypt]
Uchina	[China]
Italia; Italiano	[Italy]
Uswidi	[Sweden]
Uswisi	[Switzerland]
Ufaransa	[France]
Uhispania; Uhispaniola	[Spain]
Ureno	[Portugal]
Ujapani	[Japan]
Ujerumani	[Germany]
Uturuki	[Turkey]
Somalia; Usomali	[Somalia]
Urusi	[Russia]
Ugiriki	[Greece]
Uyahudi; Israeli; Israili	[Israel]
Uholanzi	[Netherlands; Holland]
Ubeljiji	[Belgium]
India	[India]
Korea	[Korea]
Kenya	[Kenya]
Tanzania	[Tanzania]
Uganda	[Uganda]

Msumbuji	[Mozambique]
Ushelisheli	[Seychelles]
Udachi	[Netherlands]
Bukini	[Madagascar]
Kongo	[Congo]
Serikali ya Demokrasia ya Congo	[Democratic Republic of Congo]

#### Mifano Zaidi:

Ulaya; Uropa	[Europe]
Ufini; Finland	[Finland]
Uajemi	[Iran; Persia]
Palestina	[Palestine]
Uyunani	[Palestine before 1948]
Uyorodani	[Jordan]
Uhabashi	[Ethiopia]
Norwei	[Norway]
Meksiko	[Mexico]
Kanada	[Canada]
Israili	[Israel]
Lesutu	[Lesotho]
Afrika ya kusini; Afrika Kusini	[South Africa]
Poland	[Poland]
Ukraine	[Ukraine]
Romania	[Romania]
Iraq	[Iraq]
Burundi	[Burundi]
Rwanda	[Rwanda]
Botswana	[Botswana]
Malawi	[Malawi]
Nigeria	[Nigeria]
Senegal	[Senegal]

#### Zingatia [note]

toka	[come from]
nchi	[country]
gani?	[which?; what?]

Mifano:

**4. (Wewe) Unatoka nchi gani?** [Which country

do you come from?]

a. (Mimi) Ninatoka nchi ya Marekani/Amerika.

[I come from America/U.S.A.]

b.

(Mimi) Ninatoka Tanzania / nchi ya Tanzania.

[I come from Tanzania]

c. (Mimi) Ninatoka Kenya / nchi ya Kenya. [I come from Kenya]

## Lesson 7c:

### Nationality

#### Nationality [uraia]

To refer to people's nationalities, the prefix **M-** is used for singular and **WA-** for plural.

#### A). Nationality

Mmarekani; Mwamerika	[American person]
Mwiingereza	[English/British person]
Mmisri	[Egyptian person]
Mchina	[Chinese person]
Mwitalia; Mtaliano	[Italian person]
Mswidi	[Swedish person]
Mswisi	[Swiss person]
Mfaransa	[French person]
Mhispania	[Spanish person]
Mreno	[Portuguese person]
Mjapani	[Japanese person]
Mjerumani	[German person]
Mturuki	[Turkish person]
Msomali; Msomalia	[Somali person]
Mrusi	[Russian person]
Mgiriki	[Greek person]
Mholanzi	[Dutch person]
Mbeljiji	[Belgian person]
Mhindi	[Indian person]
Mkorea	[Korean person]
Mkenya	[Kenyan person]
Mtanzania	[Tanzanian person]
Mganda	[Ugandan person]
Mmsumbuji	[Mozambican person]
Mzungu	[Caucasian person]
Mwafrika	[African person]
Mfini	[Finnish person]
Mwajemi	[Iranian person]
Myahudi	[Palestinian person]
Myorodani	[Jordanian person]

Mhabashi	[Ethiopian person]
Mnorwei	[Norwegian person]
Mmeksikana	[Mexican person]
Mkanada	[Canadian]
Mwisraeli	[Israeli person]
Msutu	[Mosotho (Lesotho) person]
Mwafrika Kusini	[South African person]
Mpoland	[Polish person]
Mkraine	[Ukrainian person]
Mromania	[Romanian person]
Miraq	[Iraqi person]
Mrundi	[Burundian person]
Mrwanda	[Rwandan person]
Mbotswana	[Motswana (Botswana) person]
Mmalawi	[Malawian person]
Mnigeria	[Nigerian person]
Msenegal	[Senegalese person]
Mshelisheli	[Seychellois (Seychelles) person]
Mdachi	[Dutch person]
Mbukini	[Malagasy (Madagascar) person]
Mkongo	[Congolese person]

### Zingatia [note]

uraia	[nationality]
mraia	[a national]
wako	[yours]
gani? kwa	[which?; what?]
hivyo	[therefore]

Mfano:

### 1. Uraia wako ni gani?

[What is your nationality?]

- a). Mimi ninatoka nchi ya **Marekani**, kwa hivyo mimi ni **Mmarekani**. [I come from the **U.S.A.**, so I am **American**.]
- b). Mimi ninatoka nchi ya **Kenya**, kwa hivyo mimi ni **Mkenya** [I come from **Kenya**, so I am **Kenyan**.]
- c). Mimi ninatoka **Kanada**, kwa hivyo mimi ni **Mkanada**. [I come from **Canada**, so I am **Canadian**.]
- d). Mimi ninatoka **Afrika**, kwa hivyo mimi ni **Mwafrika**. [I come from **Africa**, so I am **African**.]

## Lesson 7d:

### Languages

#### Languages [lugha]

All languages take the prefix -Ki-.

#### Mifano:

Kiswahili	[Kiswahili]
Kiingereza	[English]
Kifaransa	[French]

#### A). Languages

Kiingereza; Kizungu; Kimombo	[English]
Kiarabu	[Arabic]
Kichina	[Chinese]
Kiitaliano; Kiitalia	[Italian]
Kiswidi	[Swedish]
Kiswisi	[Swiss]
Kifaransa	[French]
Kihispania; Kihispaniola	[Spanish]
Kireno	[Portuguese]
Kijapani	[Japanese]
Kijerumani	[German]
Kituruki	[Turkish]
Kisomali	[Somali]
Kirusi	[Russian]
Kigiriki	[Greek]
Kilatini	[Latin]
Kiyahudi	[Hebrew]
Kiholanzi; Kidachi	[Dutch]
Kihindi	[Hindi]
Kikorea	[Korean]
Kiswahili	[Swahili]
Kiganda	[Luganda (Uganda)]
Kihausa	[Hausa (Nigeria/Niger)]
Kikongo	[Congolese (Congo)]
Kinyarwanda	[Rwandese (Rwanda)]
Kiyoruba	[Yoruba (Nigeria)]
Kizulu	[Zulu (South Africa)]
Kiwolof	[Wolof (Senegal/Gambia)]

Kibamana	[Bamana (Ivory Coast)]
Kilingala	[Lingala (Democratic Rep. of Congo)]
Kiafrikana	[Afrikaans (South Africa)]
Kishona	[Shona (Zimbabwe)]
Kiajemi	[Persian]

### Zingatia [note]

lugha	[language]
gani?	[which?; what?]
na	[and]
kingi	[a lot]
kidogo	[a little]
sana	[a lot; very much]
sema / ongea / zungumza	[speak]

Question Formation



Mifano:

**1. (Wewe) Unasema/Unaongea/Unazungumza lugha gani?**

[What language(s) do you speak?]

**a).** (Mimi) Ninasema/Ninaongea/Ninazungumza Kiingereza.

[I speak English.]

**b).** (Mimi) Ninasema/Ninaongea/Ninazungumza Kiingereza na Kiswahili. [I speak English and Kiswahili.]

**c).** (Mimi) Ninasema/Ninaongea/Ninazungumza Kiingereza, Kiswahili, na Kichina. [I speak English, Kiswahili, and Chinese.]

**d).** (Mimi) Ninasema/Ninaongea/Ninazungumza Kiingereza kingi na Kiswahili kidogo. [I speak a lot of English and a little Kiswahili.]

**e).** (Mimi) Ninasema/Ninaongea/Ninazungumza Kiingereza sana. [I speak English a lot.]

**Lesson 8:**

**Locations**

**Locations** [kutoka na kukaa/kuishi]

How to talk about location and introduce yourself in detail:



Name



Country, State, City



Current residence



School



Languages you speak

**A). Locations**

bara	[continent]
nchi	[country]
jimbo	[state]
jiji	[big city]
wilaya	[district; county]
mji	[city]
kijiji	[village]
kitongoji	[small village; hamlet]
mtaa	[neighborhood]

kisiwa	[island]
tarafa	[division]
kata	[ward]
kiunga	[suburb; outskirts]
mkoa	[province]

### Zingatia [Note]

toka	[come from]
kaa/ishi	[live; reside]
barabara	[street; road]
karibu na	[near]
lakini	[but]
kwa sasa	[for now]
katika	[at; within]

Mifano:

**5. Wewe unatoka wapi?** [Where do you come from?]

Mimi ninatoka jimbo la Kansas, mji wa Lawrence. [I come from the state of Kansas, city of Lawrence.]

**d. Wewe unakaa/unaishi wapi?** [Where do you live?]

Mimi ninakaa/ninaishi mji wa Lawrence. [I live in the city of Lawrence.]

## Sentence Formation

Mifano:

**1. Your name**

Jina langu ni / Mimi ninaitwa \_\_\_\_.

[My name is / I am called \_\_\_\_.]

**2. Where you come from and Where you live now**

Mimi ninatoka nchi ya \_\_\_\_,  
jimbo la \_\_\_\_, mji wa \_\_\_\_,  
lakini kwa sasa

[I come from the country of \_\_\_\_,  
the state of \_\_\_\_, the city of \_\_\_\_,  
but for now

mimi ninaishi/ninakaa mtaa wa \_\_\_\_,  
karibu na \_\_\_\_, barabara ya \_\_\_\_.

I live in the neighborhood of \_\_\_\_,  
near \_\_\_\_, street/avenue of \_\_\_\_.]

**3. What you study and Where**

Ninasoma \_\_\_\_ katika chuo kikuu cha  
\_\_\_\_.

[I study \_\_\_\_ at the University of  
\_\_\_\_.]

**4. What languages you speak**

Ninazungumza \_\_\_\_.

[I speak \_\_\_\_.]

Ninasema/Ninaongea Kiingereza  
kingi na Kiswahili kidogo.

[I speak a lot of English and a little  
Kiswahili.]

How to introduce yourself in detail: [Jitambulisha kwa undani:]

Jina langu ni Tyrone/Ninaitwa Tyrone. Mimi ninatoka nchi ya Amerika, jimbo la Kansas, mji wa Kansas City, lakini kwa sasa mimi ninaishi/ninakaa mtaa wa Lawrence, karibu na McDonald's, barabara ya 23rd. Ninasoma mawasiliano katika chuo kikuu cha Kansas. Ninasema Kiingereza kingi na Kiswahili kidogo.

*[My name is Tyrone/I am called Tyrone. I come from America, the state of Kansas, city of Kansas City, but now I live/stay/reside in Lawrence, near McDonald's on 23rd Street. I study communication at the University of Kansas. I speak a lot of English and a little Kiswahili.]*

## Lesson 9:

### Swahili Noun Classes

#### Noun Classes [ngeli za Kiswahili]

Nouns in Kiswahili are grouped into various noun classes because of two main reasons:

- 12. their characteristics as a noun**
- 13. Kiswahili's vowel harmony**

There are 9 noun classes in Kiswahili. Each noun class has both a singular and a plural form, to make 18 total.

<b>M-WA</b>	[A - WA]
<b>KI-VI</b>	[KI - VI]
<b>M-MI</b>	[U-I]
<b>JI-MA</b>	[LI - YA]
<b>N - N</b>	[I - ZI]
<b>U - U</b>	[U - ZI]
<b>U - U</b>	[U-U]

**KU-KU**

[KU - KU]

**PA-PA**

[PA - PA]

**MU-MU**

[MU - MU]

## Lesson 9a:

### Noun Classes

#### M-WA

<b>M-WA</b>	<b>[A - WA]</b>
KI-VI	[KI - VI]
M-MI	[U-I]
JI-MA	[LI - YA]
N - N	[I - ZI]
U - U	[U - ZI]
U - U	[U-U]
KU-KU	[KU - KU]
PA-PA	[PA - PA]
MU-MU	[MU - MU]

#### **M-WA** [A-WA]

This noun class has the following nouns:

- A).** nouns of people that start with **M-** in singular and **WA-** in plural
- B).** other nouns of people
- C).** wanyama [animals]
- D).** ndege [birds]
- E).** wadudu [insects]
- F).** samaki [fish]

## A). Nouns of people that start with M- in singular and WA- in plural

mtoto/watoto	[child/children]
mgeni/wageni	[visitor/visitors]
mfaransa/wafaransa	[French person/French people]
mjomba/wajomba	[uncle/uncle]
mke/wake	[wife/wives]
mkulima/wakulima	[farmer/farmers]
mpishi/wapishi	[cook/cooks]
msichana/wasichana	[girl/girls]
mtu/watu	[person/people]
mume/waume	[husband/husbands]
mvulana/wavulana	[boy/boys]
mzee/wazee	[elder/elders]
